




# BENKI KUU YA TANZANIA

NOTI YA SHILINGI ELFU TANO YA TANZANIA  
TANZANIAN 5000-SHILLING BANKNOTE



## ALAMA MUHIMU ZA KUTAMBUA NOTI HALALI THE MAIN SECURITY FEATURES



Alama iliyofichika kwenye noti inayoonesha sura ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na thamani ya noti ya shilingi elfu tano

*Watermark portrait of Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, with highlighted 5000*



Alama za vipande vipande zenye kuonesha thamani ya noti ya Shilingi elfu tano inapomulikwa kwenye mwanga ambapo tarakimu kamili za thamani ya noti hutokea

*Perfect see-through register when held up to the light the number 5000 appears*



Kivuli kilichofichika: Alama maalum iliyofichika yenye kuonesha thamani ya noti ya Shilingi elfu tano huonekana kuwa angavu noti inapogeuzwageuzwa

*Latent image: the number 5000 appears in shadow and turns lighter as the banknote is tilted*



Pembe zinazoparua na alama maalum zinazotambulisha thamani ya noti kwa kuipapasa kwa wenye ulemavu wa macho

*Tactile corners and distinguishing marks for the visually impaired*




Nyuzi nyembamba zenye rangi tatu zilizofichika ambazo huonekana kwa kutumia mwanga maalum wa rangi ya zambarau

*Invisible fluorescent fibres in three colours*



Alama ya usalama iliyoboreshwa kwenye utepe mwembamba inaonesha kutembea na kubadilika kwa rangi. Rangi za utepe huo zinaonesha upinde wa mistari mithili ya mawimbi yanayotembea kutoka kushoto kwenda kulia na kinyume chake, pale noti hiyo inapogeuzwageuzwa upande au juu na chini. Rangi za utepe huo zinabadilika toka rangi ya bluu kwenda zambarau. Pia, unapoelekeza kwenye mwanga, kuna maneno yanayosomeka: 'BOT 5000'

*New innovative security thread which shows a movement and a color change. When tilting the note, you can see curved lines (waves) moving from right to left and backwards. While doing this, the colour of the thread is changing from blue to violet. When holding the note against the light, in the security thread 'BOT 5000' will appear*



Alama ya wino maalum uliofichika ambayo huangaza noti ikimulikwa kwa mwanga wa rangi ya zambarau

*Invisible fluorescent ink*



Alama maalum ambayo Twiga anaonekana ndani yake, yenye rangi ya dhahabu ambayo hubadilika kuwa kijani na kurudia tena kuwa ya dhahabu noti inapogeuzwa

*Spark® - When the banknote is tilted the gold colour switches to green and back again with a rolling bar effect*



Maandishi madogo sana yaliyolala na kutuna yanayoonekana kwa kutumia vifaa maalum vya kukuzia maandishi

*Microtext lines, both flat and in relief*



Namba ya noti yenye tarakimu ambazo zinazoozongezeka ukubwa na kung'aa zinapomulikwa kwa mwanga maalum wa rangi ya zambarau

*Serial numbers whose figures increase in size, printed in fluorescent ink*



Alama ya wino maalum uliofichika ambao huonekana noti ikimulikwa kwa mwanga maalum wa rangi ya zambarau

*Invisible phosphorescent ink*